



**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

**SCHOOL BASED ASSESSMENT**

**KISWAHILI**

**SEHEMU A**

**Zoezi la 2**

**Kusoma kwa Sauti**

**Gredi ya 5-2024**

**NAKALA YA MWANAFUNZI**

Kuku ni ndege anayefugwa nyumbani. Ndege huyu ana faida nyingi. Kwanza, hutupatia nyama na mayai ambayo huimarisha afya zetu. Watu wengi hufurahia kula nyama ya kuku.

Ufugaji wa kuku ni njia ya kuimarisha pato. Unaweza kuuza kuku au mayai. Pesa zinazotokana na mauzo hayo zinaweza kutumiwa kukidhi mahitaji mbalimbali. Haya ni kama vile chakula na mavazi. Unaweza pia kuhifadhi pesa hizo katika benki zikakuletea faida.

Kuku hutupatia mbolea inayotumika shambani. Mbolea hiyo hufanya mimea kukua vyema na hivyo kufanya mazao kuwa mengi na ya kutosheleza. Mbali na hayo, mbolea ya kuku inaweza kuuzwa ili kuleta mapato. Mapato hayo yanaweza kutumika kuanzisha miradi zaidi ili kujiimarisha.